Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 8NW

ISBN 1 902059 30 -1
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412
Telephone +44 (0) 1604 765068

Email: CarlHinton@hotmail.com
Web: http:\\www.bedford-ecclesia.org.uk/Swahili

MALAIKA: WAJUMBE WA MUNGU

Angels: God's Messengers

‘Familia yote ya mbinguni na duniani’
Malaika kwa sasa ni sehemu ya lile ambalo mtume Paulo aliiita ‘ubabu wote wa mbinguni’ – Mungu Baba, Yesu mwana wa Malaika. Karibu familia itakuwa imekamilika Yesu atakaporudi mara ya pili hapa duniani na ndipo wataongezeka ‘wana wa Mungu’-Wanafunzi waaminifu wa Kristo – ambao watatawala dunia. Pamoja naye; kwa hiyo nampigia Mungu Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo magoti, ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa. (Waefeso 3:14,15,UV). Muumba anakaa katika nusu isiyoweza kuharibiwa na anaweza kuonekana kuwa yuko mbali sana na sisi mara kwa mara. Lakini ile familia ya Mungu imetoa ule utofauti uliokuwepo, na siku itakuja ambapo mwisho wa miaka Elfu moja dhambi zote zitakuwa zimeondolewa na mauti itashindwa na Mungu atakuwa yote katika wote (1 Wakorintho 15:28).

Ni jinsi gani Malaika wanavyotuhudumia?
Kwa mwamini, kule kufahamu kwamba malaika wapo kwa faida yake hii ni msaada wa kutosha. Kama tunavyoweza kuwa na Imani na daktari wa upasuaji mkubwa (ingawaje hatumuoni kwa macho kwa sababu ya dawa ya usingizi na ganzi), hivyo kuelewa kazi ya malaika ni kuwa na imani katika ulinzi wa Mungu kwetu na namna Mungu anavyohusika katika maisha yetu. Kwa hakika, kwa matendo ni kitu zaidi ya hapo. Kama kweli tuwaaminifu, tunamwomba Mungu na Mungu anajibu maombi yetu kwa pamoja kama anavyopenda yeye. Hutuma malaika wake ambaye, bila kuonekana anaamuru mazingira na hali tulizonazo, na hivyo kubadilisha maisha yetu: Hatua za mtu huimarishwa na BWANA.

Tufupishe kwa kusema, kweli malaika wanaishi na wapo kwa ajili ya kutusaidia kama tunamcha Mungu. Ukweli hautegemei yale tunayoyaona. Na hali ndilo kosa kubwa alilolifanya Bwana Khrushchev. Vitu kinavyoonekana ni ya muda tu bali visivyoonekana ni vya milele (2Wakorintho 4:18,UV).

Wakati Jeshi la mbinguni wanapotumwa kuwakusanya wateule pamoja kwa ajili ya hukumu Yesu atakaporudi, wateule wataweza kukutana na kuwaona malaika kwa mara ya kwanza Mwaliko huenda ukawa hivi, ‘Bwana amekuja anawaita!" (Yohana 11:28). Kwa sasa ni wakati wa kumwamini BWANA MUNGU na malaika zake na hivyo kujiandaa kwa ajili ya tukio hili kubwa: "Unifumbue macho yangu, ili niyatazame maajabu yatokayo katika Sheria yako". (Zaburi 119:18).

MALAIKA: WAJUMBE WA MUNGU
MAFUNDISHO YA BIBLIA KUHUSU HUDUMA YA VIUMBE WA KIROHO.
Habari imeeleza jinsi mwanaanga wa kwanza wa Kirusi aitwaye Yuri Gagarin, aliagizwa na Khrushchev waziri mkuu wa serikali ya Urusi (iliyokuwa inaitwa Soviet) ili kuangalia kama kuna malaika angani, ilikuwa ni mwezi wa April mwaka 1962. Aliporudi kutoka angani alitoa taarifa kwamba "hakuna malaika aliowaona". Na Khruschehev" alimpongeza, nilijua usingewaona kwani hakuna vitu vya namna hiyo"

Ni rahisi kudhania, kwamba kile usichokiona hakipo!.

Je, wewe unaamini kuwa malaika wapo? Je, unafahamu malaika ni nani, au wanafanya nini? Je, ni fikra za mafundi sanaa katika michoro ya dini toka karne na karne? Hivi kweli kuna kitu tunachopaswa kukifahamu? Je ni muhimu kujua kama malaika wapo?

Tuangalie Biblia
Majibu sahihi ya maswali hayo yanapatikana tu katika Biblia . hatuna chanzo kingine cha habari kinachoaminika .Biblia ni neno lenye pumnzi ya Mungu na lina maktaba ya habari inayoongelewa, kwa hiyo,ni wapi pa kuangalia?

Twende moja kwa moja kwenye biblia, kupata ushahidi unaoonekana kuhusu hawa viumbe wa mbinguni. Mfano tunaopaswa kuangalia, wa kwanza si tukio la kwanza kabisa wakati malaika wanapotajwa, lakini ni wa kutupatia mwanga. Katika nyakati zile, mnamo karne ya 8KK falme za syria na Israel zilikuwa zikipigana vita. Mfalme wa Shamu alifadhaishwa baada ya kugundua vilipo vikosi vyake vya mbele. 2wafalme 6:8-11. Baada ya kuambiwa kuwa mtoa habari alikuwa Elisha nabii wa Mungu, watumishi wake wakamteremkia Elisha na mtumishi wake katika mji mdogo ulio Kaskazini mwa Israeli. Mfalme wa Shamu alipeleka jeshi kubwa kwenda kumkamata nabii, wakaizunguka Dothani wakiwa na magari ya farasi na wapanda farasi wakati wa usiku. Mtumishi wa Elisha alipotazama asubuhi aliliona jeshi kubwa aliogopeshwa, "Ole wetu, bwana wangu tutafanyaje?"

Mtu ambaye macho yake yalifumbuliwa
Ilikuwa ni mwitikio wa asili: Walizingirwa na jeshi kubwa lililokuwa katili na adui aliye penda kutesa asiyeweza kuonyesha huruma hakika alistahili kwa njia yoyote kutishika. Lakini bwana wake yeye alitenda tofauti kabisa! Hakuwa na wasiwasi na alikwa mwenyematumaini, mwitikio wa Elisha ulikuwa! "Usiogope!" usiogope? Ninani asiyeweza kuogopa katika hali ya namna hii? Sababu ilikuwa, "walioupande wetu ni wengi kuliko walio upande wao": Alikuwa ana maanisha nini? Je, yawezekana Elisha aliweza kuona kitu ambacho mtumishi wake hakuweza kuona ? Yote yaliweza kuwa wazi wakati nabii alipomuomba Mungu.

Bwana ninakusihi mfumbue macho yake ili aweze kuona. Naye BWANA akayafumbua macho ya kijana naye akaona tazama kile kilima kilikuwa kimejaa farasi na magari ya moto yaliyo kuwa yamemzunguka Elisha pande zote" (2 Wafalme 6:17).

Elisha alikuwa mtu wa Mungu, naye BWANA alikuwa ametuma jeshi lake la ulinzi wake katika kumhudumia nabii wake. Elisha tayali alikuwa ameshaona jambo kama hilo muda kabla ya Eliya mtangulizi wake hajachukuliwa kwenda juu kutoka kwake ndipo Elisha alilia "Baba yangu, baba, yangu gari la Israeli na wapanda farasi wake (2 wafalme 2: 12).

Elisha alijua kutokana na tukio alililoliona ya kwamba malaika walikuwepo pale, mtumishi wake ambaye alikuwa hajawahi kuona alikuwa hafahamu uwezo halisi hutoka wapi. Macho yake kiroho yalikuwa yamefumbwa.

Mungu hufanya kazi kupitia Watumishi wake.
Tukio la Dothani ni ufunuo unaofundisha namna Mungu anavyo fanya kazi kwa kumlinda mtu kwa njia ya jeshi lake ambao ni wajumbe watumishi.

Walikuwa ni wengi sana kuliko magari ya fahari ya jeshi la washami wakiwa na mamlaka ya wafalme wa Wafalme aliyewatuma. Je uwepo wao pale Dothani alifanikisha lolote? Hakika ulifakisha tena kwa kuwaokoa watu wawili pamoja na mji uliokuwa makao ya watu, jeshi la washami waliingia kutoka Dothani hadi mikononi mwa wafalme wa Israel. Magari ya moto na wapanda farasi yalimfumbulia mtumishi wa Elisha kuwa walikuwa malaika wa Mungu, kwa ajili ya wale wamchao Mungu.

Kwatukio hili linafafanua jinsi mtu wa Mungu Daudi Mfalme alivyoelewa vyema na akelezea katika Zabuli zifuatazo:

"Malaika wa Bwana hufanya kituo, akiwazungukia wamchao na kuwaokoa" (34:7)

"Magari ya Mungu ni ishirini elfu, maelfu, maelfu, Bwana yumo kati yao kama katika sinai katika patakatifu". (Zaburi 68:17)

"Mhimidini Bwana, enyi malaika zake, Ninyi mlio hodari, mtendao neno lake, mkiisikializa sauti ya neno lake". Mhimidini Bwana enyi majeshi yote ninyi watumishi wake mfanyao mapenzi yake. (Zaburi 103: 20-21) "Umuhimidi Bwana … huyafanya mawingu kuwa gari lake, na kwenda juu ya mbawa za upepo, huwafanya malaika zake kuwa pepo, na watumishi wake kuwa moto wa miale. (Zaburi 104:1-4)

Jeshi la Mungu
Hapa kuna dalili zote za mambo yaliyotokea pale Dothani yanayo tupatia ujuzi kwa magari ya moto: ikiwa ni ishara ya nguvu jeshi kuzunguka uwezo mkubwa wa jeshi kuwalinda wale wamtumainio Mungu .Alama ya moto; kurudisha nyuma au kuangamiza adui. Tunakumbushwa idadi inayotia moyo, tukijulishwa ukubwa wa jeshi linalotumiwa na Mungu. Yesu alimwambia Pontio Pilato kuwa angeweza kumuomba Baba yake amletee "zaidi ya majeshi kumi na mbili ya malaika" (zaidi ya 72,000) ili kumsaidia kulipiga jeshi la Mkuu wa majeshi ya Rumi ambayo yasingekuwa na uwezo kabisa. (Mathayo 26:53). Hapa twaona pia, kuwa nguvu hizi ni nguvu za Mungu. Hawa ni malaika wake, "jeshi lake" na pia ni watumishi wake wakifanya yampendezayo.

Kwa maneno mengine ni kuwa Bwana Mungu ana mamlaka yote juu yao wanatumika kwa ubora zaidi, wao wanayo nguvu isiyo ya kawaida kuweza kukamilisha maagizo wanayopewa
Kwa ajili ya ushahidi wa tukio muhimu katika Biblia ni dhahiri kwamba wapo viumbe ambao ni Malaika na ya kuwa wao hufanya kazi kwa niamba ya Mungu na mwanadamu. Kama tunataka kujua zaidi kuhusu malaika, basi lazima tuanze na swali rahisi.

Malaika ni nani?
Neno la kiingereza "angel" linatokana na neno la kigriki "angelos" lenye maana ya "Mjumbe" katika Aganola Kale, isipokuwa kwa haya mawili, kwa Kiebrania neno "malaika" ni "malak" pia lina maana ya "mjumbe". Nabii malaki alipata jina lake kutoka neno hili. Yeye mwenywe alikuwa mjumbe na alitabiri kuhusu kuja kwa mjumbe wa agano ,Yesu Kristo (Malaki 3:1)

Ingawaje neno malaika katika Biblia, maana yake ni mjumbe, karibu mara nyingi hutumika kwa viumbe wa mbinguni, pengine hutumika kwa wajumbe ambao ni wanadamu.

Malaki mwenyewe alisema kuhani alikuwa ni mjumbe (malak) wa BWANA wa Majeshi (Malaki 2:7) na katika kitabu cha ufunuo wazee wa makanisa saba ya Asia waliitwa malaika (1:20,2:1 n.k). Lakini tunapokuta wajumbe wakifanya mambo yasiyo ya kawaida hakuna shaka hawa ni malaika wa mbinguni-wajumbe wa Mungu, walitenda kwa niaba ya Mungu na kwa niaba ya manufaa ya binadamu.

Muumbaji wa Ulimwengu.
Bwana Mungu ni muumbaji wa vitu vyote katika ulimwengu na ndiye aliyeumba malaika. Bila shaka watu wasioamini kuwa Mungu yupo na wale waaminio kuwa habari za Mungu haziwezi kupatikana hawaoni umuhimu wa malaika.Kuwa (kama wanavyoamini) kila kitu kinacho wazunguka kimetokea kwa bahati na siyo kwa kuumbwa maana watatofautiana kwa namna Mungu anavyofanya kazi. Lakin kuna ushahidi mkubwa mno wa kuwepo kwa Mbunifu Mkuu sana, siyo kwamba aliumba tu lakini pia yeye ndiye mtawala na bwana wa mpango wa dunia na wa wanadamu.

Malaika watakuwepo,wakiwa mashahidi; kwenye hukumu kuu wakati Mwana wa Adamu atakapowakiri wale wanaomkiri "mbele ya malaika wa Mungu". (Luka 12:8) kwa kuwa wao ni wavunaji wa mavuno wakati "Mwana wa Adamu awatuma malaika zake, nao watakuja kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi" (Mathayo 13: 39-41). Na baada ya hayo,watadumu katika kuwahudumia waamini wa Yesu, ambao watakuwa wamepewa uzima wa milele watakaotawala ulimwengu ule ujao wakumwakilisha Mungu hapa duniani.

Yale yote tuliyoyaona kutoka katika maandiko yanathibitisha kuwa malaika wamekuwepo tangu msingi wa ulimwengu. Ya kwamba wao leo wapo na kuwa watakuwepo katika ufalme wa Mungu hapa duniani. Wao wamepewa nguvu nyingi mno, wao wameuweka ulimwengu na tena wamefanyika daraja la tofauti kati ya BWANA MUNGU mwenye utukufu asiyeweza kuharibiwa na wanadamu hapa duniani waliojiandaa kwa kumcha Mungu. Ingawa ni kweli kuwa malaika hata wao ni hata hivyo.

Ukweli ni kwamba tangu kukamilika kwa Biblia mwishoni mwa karne ya kwanza B.K. haijawahi kutokea kile Biblia inachokiita mafumo dhahiri kama ilivyokuwa katika nyakati zilizotangulia. Kukamilika kwa Biblia kunatosheleza kuweza kutoa habari muhimu kwa ajili ya wokovu, na ndiyo maana tunatakiwa kusoma Biblia, kukubali maagizo yake na kuishi kwa imani. Imani siyo upofu wa kuamini mambo tusiyoyajua, bali Imani inajengeka katika uthibitisho Neno la Mungu na kazi yake na tena inahitajika sana katika kuamini ukweli.

Tunatakiwa kufungua macho yetu kwa uthibitisho wote unaotuzunguka kutimiliza mpango wa Mungu. Tukifanya hivyo ndipo matarajio yetu yatakuwa ya maana yanayohusu kurudiYesu Kristo kumekaribia. Lakini tunaweza kufanya zaidi ya hili. Tunaweza kusema kwa watu wale wamwaminio na wasiomfuata na kumtiiYesu na wakiwa tayari kwa ajili Ufalme, kuna msaada wa karibu wa malaika kwa kila mwanafunzi. Je, unakumbuka Zaburi ya 34? ‘Malaika wa BWANA hufanya kituo, akiwazungukia wamchao na kuwaokoa’. Kwa kuwa macho yetu yana mpaka wa kuweza kuona hatuwezi kumuona malaika mlinzi, lakini pale malaika yupo hapo, je, uko tayari kuamini haya?

Je, malaika ni walinzi?
Na kwa kuwa malaika wanafanya kazi kwa niaba ya wanaotafuta ili kuwa watoto wa Mungu, watoto wake wa kiume na wa kike – watu wengi kuuliza kama kuna kiumbe malaika ‘walinzi’. Wakati Petro alipofunguliwa na malaika kutoka katika Gereza (Matendo 12:7-15) na akafika mlango wa nyumba ambayo walikuwemo waamini walio kutania humo; hawakuweza kusadiki kama ni Petro mwenyewe lakini walisema, ni malaika wake’. Lakini kabla ya hapo, Yesu alikuwa amekwishawaambia wafuasi wake kuwa walio wapole wenye kutii kwa kuamini kama mtoto alivyo. Wanaomnyenyekea Mungu wapate huduma ya watumishi wake. ‘Kwa kuwa malaika wao siku zote huutazama uso wa Baba yangu aliye mbinguni’. (Mathayo 18:10). Hivi ni vielelezo vya muhimu kuonyesha kuwa Mungu humlinda kila mtu kumwokoa anayeteswa na yupo tayari kuwasaidia wote wamchao Wanafunzi wa Yesu hawa huachwa na mashaka wakati wanaposoma waraka kwa Waebrania.

Sura za mwanzoni zinadhihirisha namna Mungu alivyokuwa akiwasiliana na watu, jinsi gani malaika walivyowatumishi wake na kwa namna Yesu ambaye ni Mwana wa Mungu amefanyika bora kuliko malaika na kustahili kupewa heshima na wao. Vile vile wale wote wanaofanyika wana wa Mungu na hasa wale watakaoingia katika ufalme na kuwa wafalme katika ufalme wa Mungu ule ujao watakuwa wakuu kuliko malaika. Katika sura ya 1 mwandishi anasema kwamba Mungu ambaye alisema zamani kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi (Kwa mfano, kwa njia ya malaika waliopokea neno toka kwa Mungu na kulipeleka kwa mababu na manabii). Lakini kwa sasa anasema moja kwa moja katika mwana wake, ‘ambaye ni chapa ya nafsi yake Mungu akiwa amefanyika bora kupita Malaika kwa kadri ya jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko wao’ Mwana ni mkuu kupita Watumishi. Hata sasa mwandishi anasema, malaika wanaendelea kufanya kazi zao.

‘Na kwa habari za malaika asema, Afanye malaika wake kuwa pepo, na watumishi wake kuwa miali ya moto….Je! hao wote si roho watumikio wakitumwa kuwahudumu wale watakaourithi wokovu? (Waebrania 1:7,14,UV)

Hii ilikuwa habari isiyo ya kawaida kwa kuwa Mariamu alikuwa hajaolewa. Hakuna neno lisilowezekana kwa Mungu! Yusufu, mmewe mtarajiwa, naye pia alipokea ujumbe wa malaika uliomsihi namna ya kufanya kulingana na tukio hili la kipekee.

Wakati Yesu alipozaliwa Bethlehemu, ishara ya kuzaliwa kwake ilikuwa ishara ya uthibishto wa utukufu wa Mungu ulioonekana kwa wachungaji:
"Malaika wa Bwana (yawezekana kuwa Gabrieli?) aliwatokea na utukufu wa Bwna ukawang'arizia pande zote, wake ukiwa na hofu kuu Mara walikuwepo pamoja na huyo malaika, wingi wa jeshi la mbiguni, wakimsifu Mungu na kusema, Atukuzwe Mungu juu mbinguni na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia (Luka 2:9-14 U.V)

Malaika Wanahubiri Injili
Katika tukio hili la utukufu tunaona kwanza kazi maalumu ya malaika mmoja, akitokea katika utukufu wa Mungu, pili kundi kubwa la malaika wenzake wanao husika katika kutimia kwa ahadi wote, wakipatana, wakitangaza utukufu wa Mungu mwenyenzi, na tatu, tangazo la habari njema ya kuja kwa ufalme wa Mungu hapa duniani na amani kwa watu wote wamchao, na "wanao tetemekea neno lake" unaochochea hiki kilikuwa kichocheo kinachoimarisha uthibitisho wa jinsi Munjgu anavyojulisha mapenzi yake kwa njia ya wajumbe wake.

Yesu alipokua alifahamu kabisa kazi walizozifanya Malaika katika maisha yake. Tunasoma kwamba mwisho wa jaribu lake kwa muda wa wiki sita, hali akiwa pweke, katika Yyudea nyikani, alipokuwa ana njaa na akiteseka kutokana na ugumu wa jaribu, alihitaji msaada na kuwa pamoja na wengine, "wakaja Malaika wakatumikia" (Mathayo 4:11). Tena katika bustani Gethsemane, malaika walikuwepo pale, marafiki ambao Yesu alikuwa na fikiria ya aina moja na wakishiriki mawazp. Na ambapo hata wanafunziwake wa karibu wasingestamili hali ya shiniko, hakika Malaika walikuwa rafiki zake kweli?

Malaika katika mambo ya ulimwengu.
Wakati yesu aliposali "ufalme wako nje, mapenzi mbinguni" alikuwa akithibitisha ubora wa kazi za malaika kuhusu vitu vyote ulimwenguni. Ni wao ambao, kwa uwezo waliopewa na Mungu, wameweka nyota na sayari katika mpangilio mzuri kabisa. Wakati Yesu atakaporudi tena mpangilio wa dunia utakuwa mzuri kama huo. Kwa wakati Daniel alisema " aliye juu anatawala katika ufalme wa wanadamu" (Daniel 4:17), nay kuwatumia watumishi wake malaika kuyatenda mapenzi yake katika mataifa. Wao wanaonyesha tabia yake; kwa mfano wao ni "macho yake" malaika mara moja anamwelezea malaika mwenzake kwa Nabii Zekaria kama " hawa ndio BWANA aliowatuma, waende huko na huko duniani na macho ya BWANA yapiga mbio huko na huko duniani (Zekaria 1:10; 4;10 uv). "macho" hapa yanaonekana kuwa maelezo yanayofaa wakati malaika wanapokuwa katika ulinzi!

Malaika wakati wa kurudi mara pili ya Kristo.
Kwa uwezo walionao, malaika hawafahamu kila kitu. Kwa mfano, ufahamu wao kuhusu wakati halisi ambapo Yesu atarudi unampaka; kwa kuwa Yesu alisema, "walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye hata malaika walio mbinguni wala mwana, ila baba peke yake (Mathayo 24:36). Lakini ni kweli kwamba wao ni wahusika sana katika tukio hili la kurudi mara ya pili na kuuweka ufalme wa Mungu. wao hawatakuwa watendaji waku nguvu zao ambazo ni kubwa mno na uwezo zitakuwa dhahiri wakati.

"Bwana Yesu atafunuliwa kutoka mbinguni pamoja na malaika Wa uweza wake, katika mwali wa moto huku akiwalipiza kisasi wao wasiomjua Mungu, na wao wasioitii Injili ya Bwana wetu Yesu Kristo yeye atakapokuja ili kutukuzwa katika watakatifu wake". (2 Wathesalonike 1: 7-10)

"Ndipo mataifa yote ya Ulimwengu watakapoomboleza, nao watamuona akija juu ya mawingu ya mbinguni pamoja na nguvu na utukufu mwingi. Naye awatuma malaika zake pamoja na sauti kuu ya parapanda, nao watawakusanya wateule wake toka pepo nne, toka mwisho huu wa mbingu mpaka mwisho huu". (Mathayo 24:30,31)

Kwa kuwa msaada wa mbinguni utakuwepo pamoja na Yesu wakati wafu watakapo fufuliwa: "Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza…" (1 Wathesalonike 4: 16 UV)

Kwa msomaji mwenye kusadiki ataelewa kwa nini Muumba huelezea makusudi yake kwa viumbe wenye ufahamu ya kuwa yeye ndiye Muumba.

Bwana Mungu wakati wote yupo na yeye siku zote atakuwepo, na ndiyo maana biblia humwelezea kuwa yeye ni wa milele na milele (Zaburi 90:2). Yeye ni Mungu aliye hai (ni tofauti kabisa na wote wanaoitwa miungu) chanzo cha nguvu zote ,uzima wote, na mambo yote yaliyo ya muhimu kwa ajili ya kuendelea kwa uzima. Katika uumbaji wa mfumo wa jua, nyota, sayari zote na vitu vyote vilivyo angani. Ameiweka dunia peke yake kwa makusudi maalumu, kwa makusudi ya kwamba iweze kuwa sehemu ya viumbe hai wenye kuweza kuuonyesha utukufu wake na kudhihirisha sifa zake. Na dunia yote na utukufu wangu itakuwa imejawa (Hesabu 14:21) ni ahadi yake. Ingawaje yeye ni Roho mwenye nguvu, yeye siyo aina ya mashine inayojiendesha.

Mungu hakuumba mtu aliyekama mashine kwa ajili ya kuishi kulingana na maisha ya duniani, bali, yeye alipenda kuanzisha kizazi kilichopaswa kukubali mapenzi yake kuanzia mwanaume na mwanamke ambao wangemnyenyekea na kumtii yeye.

"BWANA asema hivi, mbingu ni kiti changu cha enzi, na dunia ni mahali pa kuweka miguu yangu,……. Lakini mtu huyu ndiye nitakaye mwangalia mtu aliye mnyonge, mwenye roho iliyopondeka na atetemekaye asikiapo neno langu" (Isaya 66:1,2)

Kwa nini Mungu aliwaumba malaika?
Yeye Muumba ni mwenye uweza na utukufu hata asiweze kukaribiwa na mwanadamu katika namna alivyo. Yeye peke yake asiyepatikana na mauti, amekaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa, wala hakuna mwandamu aliyemwona wala anaweza kumwona. (Timotheo 6:16). Kwa kuwa malaika wao hawana upungufu kwa hiyo wanatenda kwa ajili ya Mungu wakimwakilisha yeye wanapowasiliana na wanaume na wanawake. Wao hufanyika faraja kati ya ufa mkubwa kati ya utukufu na ukamilifu wa Mungu wa Mbinguni na dhambi damu anayekufa katika sayari hii. malaika wao ni wa milele (yaani, hawafi). Umilele wao ni wa namna moja na ule Yesu aliounena wakati aliposema: Lakini wale wahesabiwao kuwa wamestahili kuupata ulimwenngu ule na kule kufufuka katika wafu, hawaoi wala hawaolewei; wala hawawezi kufa tena; kwa kuwa huwa sawa sawa na malaika nao ni wana wa Mungu kwa vile walivyo wana wa ufufuo (Luka 20:35,36). Lakini Yesu alisema hivyo, kwa namna moja na Malaika (watoto au "wana" wa Mungu) wanaishi milele na ni wa jinsia moja,kwa hiyo pia wale watakaoitwa "wana" na mabinti wa Mungu wakati Yesu atakaporudi watawezakuishi milele na hawataoa au kuolewa

Wana wa Mungu
Wakiwa wameumbwa na Mungu , malaika wanaitwa "wana wa Mungu" Mungu anamwelezea baba mkuu Ayubu, katika kuelezea jambo hili la uumbaji wa nchi na kumuuliza. Ulikuwa wapi nilipoiweka misingi ya nchi?

Misingi yake ilikazwa juu ya kitu gani? Au ninani aliyeliweka jiwe lake la pembeni, hapo nyota za asubuhi zilipoimba pamoja na wana wote wa Mungu walipopiga kelele kwa furaha? (Ayubu 38:4-7)

Hawa wana wa Mungu walikuwepo wakifanya kazi kwa niaba ya Mungu mweza wa yote. Yeye muumba aliwaagiza na kazi ikatendeka. Kama zaburi ya 33 isemavyo, maana yeye alisema ikawa, yeye aliamuru ikafanyika (33:9). Yeye BWANA alisema neno nao malaika wakatekeleza, na kazi waliyofanya waliifanya "vyema" na ndiyo sababu imeandikwa kwa kurudiwa mara nyingi katika Mwanzo 1. Kusema, " Mungu akaona kuwa vyema" kwa sababu, "mjumbe mwaminifu huwaburudisha bwana zake nafsi zao, wamtumao" (Mithali 25:13)

Mwanadamu aliumbwa mdogo kuliko Malaika wakati mtu wa kwanza alipoumbwa, malaika walimpatia umbo linalofanana nao;"Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, na kwa sura yetu……. Kwa hiyo Mungu alimuumba, mwanamme na mwanamke aliwaumba (Mwanzo 1:26-27).Hili halimaanishi kuwa mzazi wa kwanza wa wanadamu alikuwa na umbo la asili sawasawa na malaika,kwa kuwa malaika wao waliumbwa ili waishi milele. Adamu na Eva hawakuwa ili wasife; wao walitenda dhambi, na wao wakapatwa na kifo kama adhabu ya dhambi. Na hiyo ndiyo sababu watu wote tangia hapo wamekuwa wanakufa. Ukweli kuwa mtu aliumbwa kwa mfano wa malaika ni kuelezea upeo wa mwisho wa kusudi la Mungu kwa viumbe wake.

Katika zaburi ya 8, ni zaburi inayotujulisha kuhusu uumbaji wa nchi jinsi ulivyo. Hapa tunajulishwa kwamba nafasi ya mtu katika kuumbwa ni ya chini sana kuliko ile ya malaika:

Mtu ni kitu gani hata umkumbuke?…… umenifanya mdogo punde kuliko malaika; umemvika taji ya utukufu na heshima. (Zaburi 8:4,5)

Agano la Kale linanukuu fungu hili la maneno, nalo linatujulisha kwamba watu wote akiwemo na Bwana Yesu mwenyewe aliumbwa mdogo punde kuliko malaika, "sababu ya maumivu ya mauti" (waebrania 2:9) Malaika hawafi, lakini wanaume na wanawake hufa, na hata Yesu , mwana wa Mungu, alikuwa wa kufa, lakini sasa alipokea utukufu na heshima kama malipo yake "nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani" (Mathayo 28:18)

Mwenye nguvu nyingi.
Zaburi ya 8 ni msaada kwa kuwa neno la asili hapa la ‘angel’ siyo malak (messenger) ila elo him, ni neno la uwingi lenye kumaanisha mwenye uweza (au mwenye nguvu nyingi) mmoja’. Neno elohim ni neno la kiebrania ambalo mara nyingi linamwelezea jinsi Mungu alivyo katika agano la Kale. Hata hiyo kuna mambo yaliyo ya pekee katika neno hili, ni muhimu tunaposoma Agano la Kale kufahamu kuhusu fungamano la nia kati ya Mungu na wale wajumbe wake.

Hili huwa utangulizi muhimu, namna malaika wanavyofanya kazi zao. Wakiwa ni wajumbe wanaotumwa kumwakilisha Mungu, wao huchukua jina lake na kuyatekeleza mapenzi yake. Wao wana utukufu kwa kuwa Mungu ni mwenye utukufu. "BWANA ni mwenye enzi nao malaika ni wana wa mwenye enzi" (Zaburi 89:6). Jina la heshima au cheo kingine cha Mungu ni "BWANA wa majeshi" kwa sababu kama tulivyoona. Mungu ndiye mwenye kutawala na Bwana wa Majeshi.

Tumeona kwamba malaika wanatekeleza amri ya BWANA Mungu, wao walihusika katika uumbaji wa nchi, wanatenda wakiwa wajumbe na wanatenda katika jina la BWANA. Na sasa tutaona jinsi walivyoongoza,kufikisha na kuwalinda watu wa Mungu, Taifa la Israeli.

Historia kuhusu malaika katika Agano la kale.
Kuna tukio la muhimu lililotokea kuhusu Abrahamu , "aliyewakaribisha malaika pasipo kujua" (waebrania 13:2). Siku moja "BWANA" alimtokea katika mialoni ya Mamre, alipokuwa amekaa katika mlango wa hema yake mchana wakati wa hari, akainua macho yake, akaona na tazama watu watatu wamesimama mbele yake" (Mwanzo 18:1,2). Watu hao walipewa chakula, lakini walibadilika na kuwa malaika,walikuwa wamefika kwa kazi mbili; kwanza kumjulisha Sara, kwamba atamzaa mwana, na pili, kumjulisha kuhusu miji ya sodoma na Gomoroa, jinsi itakavyoangamia kutokana na dhambi zao. Baada ya chakula, Abrahamu aliondoka hemani mwake, akawasindikiza. Wawili kati yao wakaelekea sodoma, ambapo malaika wawili walifika Sodoma jioni, na mtu mwingine anayetajwa kuwa ni "BWANA" aliyekuwa akisikiliza maombi ya rehema ya Abrahamu kwa ajili ya mji ule ambapo Lutu mtoto wa nduguye alikuwa akiishi.

Yakobo, ambaye alikuwa mjukuu wa Abrahamu alishuhudia waziwazi baadhi ya malaika. Katika kukimbia kwake kwenda Padani-aram akiikimbia hasira ya Esau nduguye ndipo alipoota ndoto ambapo aliwaona malaika wa Mungu "wakipanda na kushuka" ngazi imesimamishwa juu ya nchi na ncha yake ya fika mbinguni (Mwanzo 28:12)

Huu ni mfano halisi wa namna ya mawasiliano kati ya mbinguni na duniani yalivyoimarishwa na kwa jinsi malaika wanavyowalinda wale walioweka tumaini lao kwa Mungu.
Hatimaye, Yakobo aliweza kurudi nyumbani kwao miaka 20 baadaye, lakini alikimbia kwa hofu ya kuonana na Esau ambaye alikuwa akimjia akiwa na watu 406. Faraja na ulinzi wa Mungu ulikuwepo tena pole. Malaika wa Mungu walikutana naye, na Yakobo alipowaona alisema hili ni jeshi la Mungu (Mwanzo 32:12) Hata hivyo kuamini kuwapo na mamlaka za malaika hakuondoi sehemu ya matarajio yetu katika kutumia viungo vyetu vya mwili; Yakobo alipojua kuwa "mtu" yule aliyekutana naye na akashindana naye mweleka katika hali ya uchungu usiku kucha alifahamu kuwa mshindani wake alikuwa malaika, aliyempatia Yakobo heshima kwa kulibadilisha jina lake na kuwa "Israel" ikimaanisha " mwana wa kiume wa mfalme" . Yakobo akatangaza kuwa, nimemuona Mungu uso kwa uso, na nafsi yangu imekoka (Mwanzo 32:24-30)

Malaika aliyelichukuwa jina la Mungu.
Wakati wana waisraeli walipokombolewa kutoka utumwani nchini Misri na kuanza safari yao ya kurudi katika nchi ya ahadi, alikuwa ni Malaika wa Mungu aliyeongoza makabila yote ya Israeli Kutoka 14:19). Baada ya miezi kadhaa walifika mlima Sinai, mkutano wa watu milioni mbili walikusanyikia chini ya mlima mtakatifu (mahali musa alipomwona malaika wa Mungu katika kichaka kilichokuwa kinawaka moto) na alitishwa na tukio hili la nguvu za Mungu katika ngurumo na radi, moshi moto na tetemeko la ardhi. Musa akaitwa apande juu ya mlima uliokuwa nautukufu wake wote uliokuwa umetoka kwa Mungu, na mbao za mawe zenye amri muhimu kumi "zilizoandikwa kwa kidole cha Mungu" Uasi wa waisraeli wakati Musa alipokuwa hayupo pamoja nao, ndio hasa uliosababisha kuvunjwa kwa agano ambalo Mungu alikuwa amelifanya na taifa hili; lakini hata hivyo Musa akawa mwombezi na kumsihi BWANA MUNGU mwenyewe awaongoze watu hao, katika njia yao ya kanaani. Naye BWANA alijibu kwamba yeye mwenyewe hatakweda, bali; Tazama, mimi namtuma Malaika aende mbele zakeo, ili akulinde njiani na kukupeleka mpaka mahali pale nilipolutengenezea. Jitunzeni mbele yake msikilize sauti yake msimtie kasirani, maana hatawasamehe makosa yenu kwa kuwa jina langu limo ndani yake. (Kutoka 23; 20,25)

Malaika aliyekuwa uso wa Mungu
Tazama mamlaka aliyopewa malaika huyu, Mungu aliweka jina lake ndani ya mjumbe; malaika angeweza kuwalinda safarini lakini wamsikilize vinginevyo angewaangamiza. Hata hivyo BWANA mwenyewe "asingekwenda kati yenu" lakini " uso wake" utakwenda pamoja nao. Kutoka 33:3,14. Nguvu za Mungu, utukufu na mamlaka yote angevalishwa malaika huyu. Haina maana kuwa watu wangemuona malaika, bali uthibitisho wa kuwepo kwake ungekuwa ndani ya nguzo ya wingu mchana na katika nguzo ya moto ambayo ingekuwa juu ya masikani usiku. Kama wangalikuwa na mcho ya kuona wangefahamu kuwa alikuwemo mle bali walijali sana mambo yao. Ni Musa na Kuhani Mkuu wakiokuwa wakiikaribia maskani kuliko watu wote. Na hakuna mtu yeyote, isipokuwa kuhani mkuu ambaye aliingia mara moja kila mwaka (siku ya upatanisho) aliweza kupata maarifa mengi kutokana na kuona utukufu wenye mng’ao uliokuwa unakaa katikati ya mabawa ya makerubi wa dhahabu waliokuwa juu ya sanduku lililokuwa patakatifu pa patakatifu ndani ya maskani.

Makerubi wametajwa kwa mara ya kwanza wakati Adamu na Hawa walipofukuzwa kutoka Edeni ndio walioilinda njia ya kwenda kwenye mti wa uzima (Mwanzo 3:24) nao hao makerubi walitengenezwa kutokana na dhahabu juu ya sanduku kuonyesha ulinzi wa Mungu na uangalifu.

Tena, wakati Musa alipokuwa juu ya mlima Sinai alipenda kuuona uso wa Mungu mwenyewe, lakini hakuruhusiwa kuuona isipokuwa kushuhudia utukufu wa BWANA ulipokuwa ukipita "huwezi kuniona uso wangu, maana mwanadamu hataniona akaishi" (Kutoka 33:20). Naye Bwana Yesu alithitisha hili aliposema " hakuna mtu yeyote aliyemwona mungu wakati wowote" (Yohana 1:18) Kwa hiyo malaika walileta ujumbe wa Mungu kwa wanaume na wanawake ambao vinginevyo mwanadamu mwenye dhambi asingeweza kuupokea kwa sababu Mungu ni Mtakatifu.

Malaika na Majina yao.
Lakini kuna wakati malaika walipewa majina; kwa mfano "Mikaeli" alikuwa ni "jemadali mkuu asimamaye upande wa wana wa watu wako (Israel)" (Daniel 12:1). Na bila shaka kati ya mifano inatoa elimu sana ya kuonekana kwa dhahiri malaika ni ule wa malaaika ambaye jina lake ni "Gabriel". Huyu alitumwa mara mbili kwa nabii Daniel. Katika tukio la pili ni wakati Danieli alipokuwa akiomba na Gabrieli akarushwa upesi akanigusa….. akaongea nami, aliendelea kutabiri wakati wa kuja kwa mara ya kwanza kwa Masihi Yesu Kristo (Daniel 9: 21-27). Kwa hiyo wayahudi walikuwa wakitazamia sana wakati wa kuzaliwa kwa Yesu kristo kulipokaribia ;kuonekana dhahiri kwa Grabriel tena kulizidishia matazamio kwanza kwa Zakaria kuhani aliyekuwa zamu hekaluni na kisha kwa Mariamu aliyekuwa ameposwa na Yusufu. Kwa Zakaria , malaika akamwambia "mimi ni Gabrieli nisimamaye mbele za Mungu, nami nimetumwa niseme nawe" (Luka 1:19). Tunaona kuwa Malaika anao uwezo wa kusimama mbele ya uso wa BWANA, jambo ambalo wanadamu hawawezi, hivyo Malaika hutumwa kufanya yote yaliyo mapenzi ya Mungu. Hapa ujumbe wake ilikuwa kutangaza muujiza wa kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji.
Miezi sita baadaye,Gabrieli alimtokea Mariamu;ambaye alikuwa ni wa ukoo wa Mfalme Daudi.Maombi yake Mariamu;malaika alisema ,uliyepewa neema na Mungu,nawe utakuwa mama wa Masihi anayetarajiwa. Gabriel alimwambia kuwa atapata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu na mtoto wake ataitwa Yesu, Mwokozi, naye atakuwa Mwana wa Mungu na atakalia kiti cha enzi cha Daudi (Luka 1: 26-33).

Mfasiri: Jonathan Nkombe
Mwandishi: Carl Hinton

Tena kuakupatikana:

1 902059 00 - X	Matayarisho ya Ubatizo
1 902059 01 - 8	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 1-4
1 902059 02 - 6	Ukimwi
1 902059 03 - 4	Mshitaki Wenu Ibilisi
1 902059 04 - 2	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 5-8
1 902059 05 - 0	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 9-11
1 902059 06 - 9	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 12-15
1 902059 07 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 16-19
1 902059 08 - 5	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 20-23
1 902059 09 - 3	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 24-27
1 902059 10 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 28-31
1 902059 11 - 5	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 32-36
1 902059 12 - 3	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 37-40
1 902059 13 - 1	Ufunuo Mlango wa Kwanza
1 902059 14 - X	Ni kweli Yesu Kristo alishuka kutoka mbinguni?
1 902059 15 – 8	Nyimbo za ndugu wa Kristo
1 902059 16 – 6	Ufunuo Mlango wa Pili
1 902059 17 – 4	Katiba ya Makanisa
1 902059 18 – 2	kitabu-mwalimu wa kristadelfiani
1 902059 19 – 0	Kuanzisha Kristadelfiano (CBM) Eklesia
1 902059 20 – 4	Waraka wa mtume Paulo kwa Wagalatia sura moja
1 902059 21 – 2	Ni kwa sababu gani Mungu anaruhusu mateso?
1 902059 22 – 0	Ufufu Kwa Hukumu
1 902059 23 – 9	Waraka wa mtume Paulo kwa Wagalatia sura mbili
1 902059 24 – 7	Waraka wa mtume Paulo kwa Wagalatia sura tatu
1 902059 25 – 5	Waraka wa mtume Paulo kwa Wagalatia sura nne
1 902059 26 – 3	Waraka wa mtume Paulo kwa Wagalatia sura tano
1 902059 27 – 1	Waraka wa mtume Paulo kwa Wagalatia sura sita
1 902059 28 – X	Fungu Lako Katika Ahadi za Mungu
1 902059 29 – 8	Kuishi Katika Ile Kweli
1 902059 30 – 1	**MALAIKA: WAJUMBE WA MUNGU**